

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO
KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA HALMASHAURI MKUU – ROMBO**

TAREHE 22/10/2021.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

- | | |
|--|-------------------------------------|
| 1. Mh. Diwani Gilbert A. Tarimo | - Mwenyekiti |
| 2. Mh. Diwani Abdallah B. Mbago | - Mjumbe |
| 3. Mh. Diwani Eng. Mathias A. Benedict | - Mjumbe |
| 4. Mh. Diwani Issack S. Tarimo | - Mjumbe |
| 5. Mh. Diwani Albin S. Massawe | - Mjumbe |
| 6. Mh. Diwani Felichesmi A. Oisso | - Mjumbe |
| 7. Mh. Diwani Prisila Y. Shayo | - Mjumbe |
| 8. Mh. Diwani Martina P. Gabusa | - Mjumbe |
| 9. Mh. Diwani Athuman M. Kimario | - Mjumbe |
| 10. Mh. Diwani Clara J. Gwandu | - Mjumbe |
| 11. Mh. Diwani Msarie S. Lyimo | - Mjumbe |
| 12. Ndg. Judith P. Mahende | - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji -Katibu |

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA/KWA TAARIFA

1. Mh. Prof. Adolf F. Mkenda -Safarini kikazi.

MAAFISA WASHAURI WALIOHUDHURIA

- | | |
|---------------------------------|---|
| 1. Ndg. Robert P. Muna | - Kaimu Afisa Utumishi na Utawala (W) |
| 2. Ndg. Chrispin P. Mng'anya | -Afisa Mipango naTakwimu (W) |
| 3. Eng. Boniface Vedasto | - Kaimu Mhandisi wa ujenzi (W) |
| 4. Ndg. Rashid O. Kimweri | - Kaimu Afisa Manunuzi (W) |
| 5. Ndg. Adam R. All | - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 6. Ndg. Emmanuel Alphonse | - Kaimu Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu (W) |
| 7. Ndg. Consolata Massawe | - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 8. Dr. Nestory Lucas Ita | - Kny; Mganga Mkuu (W) |
| 9. Ndg. Zema H. Jamal | - Kny; Kaimu Katibu Msaidizi TSC |
| 10. Ndg. Charles D. Mganga | - Afisa Uchaguzi (W) |
| 11. Ndg. Arbogast Z. Mhumba | - Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira (W) |
| 12. Ndg. Bertha Joakim | - Kaimu Afisa Nyuki (W) |
| 13. Ndg. Jane B. Ngaeje | - Afisa Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi (W) |
| 14. SR. Felista M. Bukori | - Afisa Kero (W) |
| 15. Ndg. Abel M. Mushi | - Kny; Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria (W) |
| 16. CPA. Victoria S. Msuya | - Mweka Hazina (W) |
| 17. CPA. Gasto Casmir | - Mhasibu |
| 18. Ndg. Masudi Iddi Mwinyimvua | - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika (W) |
| 19. Ndg. Eulagio M. Daudi | - Afisa Usafirishaji (W) |
| 20. Ndg. Veronica Sway | -Afisa Utumishi na Utawala |
| 21. Ndg. Ernest Kileo | -Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 22. Ndg. Thomas B. Zakayo | - Kaimu Afisa Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Mkuu. |

SEKRETARIETI

- | | |
|---------------------------|----------------------|
| 1. Ndg. Patricia Marandu | - Mwandishi wa vikao |
| 2. Ndg. Wilehard K. Komba | - Mwandishi wa vikao |

AGENDA; NA. 21/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao baada ya kuona akidi ya wajumbe imetimia, ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa ni kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za kipindi cha mwezi Septemba 2020/2021. Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:45 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe na wataalam wa Halmashauri kwenye kikao hicho.

AGENDA; NA. 22/2021/2022: KURIDHIA AGENDA.

Agenda zifuatazo zilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe;

- i. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita tarehe 24/09/2021.
- ii. Yatokanayo na kikao kilichopita cha tarehe 24/09/2021.
- iii. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha Julai – Septemba 2020/2021.
- iv. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha robo ya pili Julai-Septemba 2021/2022.
- v. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwezi Julai – Septemba 2021/2022.
- vi. Taarifa ya Madeni ya Wazabuni Hadi Septemba 2021.
- vii. Taarifa ya Manunuzi kwa kipindi cha Julai – Septemba 2021/2022.
- viii. Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani kwa kipindi cha Julai – Septemba 2021/2022.
- ix. Taarifa ya kesi Mbalimbali kwa kipindi cha Julai – Septemba 2021/2022.
- x. Taarifa ya Kero za wananchi kwa kipindi cha Julai – Septemba 2021/2022.
- xi. Taarifa ya ukarabati na ujenzi wa Kituo cha Afya Mkuu.
- xii. Taarifa ya mapendekezo ya uteuzi wa wenyeviti na makatibu wa mabaraza ya kata
- xiii. Taarifa ya mzabuni aliyeshinda zabuni ya uzoaji taka Ngumu, zabuni NA.LGA/044/HQ/2021/2022/NC/07 LOT 1 & LOT 2 na zabuni ya ukusanyaji ushuru wa maegesho stendi ya Mkuu, Holili na Tarakea
- xiv. Taarifa ya mpango wa kuinua uchumi na huduma za kijamii baada ya UVIKO 19 (tanzania COVID 19 socio-economic recovery and response plan (TCRP)
- xv. Taarifa ya vikundi vilivyopitishwa na Kamati ya Mikopo robo ya kwanza Julai-Septemba 2021/2022.
- xvi. Taarifa za Kiutumishi.
- xvii. Taarifa Mbalimbali.
- xviii. Kufunga kikao.

AGENDA; NA. 23/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 24.09.2021

Muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 24/09/2021 ulipokelewa na kukubaliwa kisha Mwenyekiti na Katibu waliweka saini kuwa kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

AGENDA; NA. 24/2021/2022: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 24.09.2021

1. Kupeleka fedha iliyotengwa kwenye bajeti Masekini

Kiasi cha **Tshs.10,000,000/=** iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio kwenye dampo la zamani iende kutekeleza shughuli katika eneo linalopendekezwa kuwa dampo (Masekini).

Barua yenye Kumb. Na. HWR/M20/10/125 ya tarehe 12/10/2021 imeandikwa kwa Mkurugenzi Mtendaji kuomba fedha hizo zielekezwe eneo la dampo jipya la Masekini. Tathmini inafanyaika kubaini gharama halisi za ujenzi huo.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili.

Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe waliagiza kuwa jitihada zifanyike ili dampo hilo liweze kuhama.

2. Taarifa ya Madeni ya Halmashauri

Taarifa ya madeni yote ya Halmashauri iwe inaambatanishwa kwenye taarifa ya fedha ili mwenendo wake uweze kujulikana kwamba Halmashauri ilikuwa inadaiwa kiasi gani na kiasi gani kimebakia kwa madeni ya muda mrefu na muda mfupi.

Mweka Hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji alitolea ufanuzi hoja hiyo na kuwaeleza wajumbe kuwa taarifa hiyo iliambatanishwa kwenye Kabrasha.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili.

Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe hawakuridhika taarifa hiyo kwa kuwa haijaka sawa na maagizio yaliyotolewa hivyo waliagiza taarifa hiyo ikaandaliwe upya na kuwasilishwa kwenye kikao kijacho.

AGENDA; NA. 25/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA KWA KIPINDI CHA JULAI –SEPTEMBA 2020/2021

Afisa Utumishi na Utawala kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Idara hiyo kwa kipindi cha robo ya Kwanza (Julai-Septemba) 2021/2022 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa Idara imetekeliza shughuli zifuatazo:-

1. Kuwaondoa watumishi kumi na tisa (19) kwenye orodha ya malipo ya mishahara kwa sababu mbalimbali kama ifuatavyo;
 - (a) Kustaafu kazi kwa Mujibu wa sheria watumishi Kumi na sita (16).
 - (b) Watumishi watatu (03) kufariki dunia
2. Kuendelea na ukamilishaji wa zoezi la kupandisha vyeo watumishi ambapo hadi kufikia mwezi Septemba 2021 zoezi hilo liliokamilika na jumla ya watumishi 1182 walipandishwa vyeo na tayari wameshapata mishahara ya vyeo vypa.
3. Kuratibu zoezi la kupokea watumishi arobaini na nane wa ajira mpya walioajiriwa mwezi Julai 2021 ambapo zoezi hilo lilikamilika pamoja na taratibu za kukamilisha ajira zao hadi kufikia mwezi Agosti 2021. Aidha aliendelea kueleza kuwa watumishi hao tayari walikuwa wameingizwa kwenye orodha ya malipo ya mishahara.
4. Kusimamia Ufanyakaji wa vikao vya kisheria katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji.
5. Kusafisha taarifa za watumishi kwenye mfumo.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili.

Wajumbe walishauri kuwa Vijiji ambavyo havina watendaji ni vizuri viwekwe kwenye mpango ili viombewe watendaji Serikalini.

AGENDA; NA. 26/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI JULAI-SEPTEMBA 2021/2022

Kaimu Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai-Septemba 2021/2022 ambapo aliwaeleza wajumbe kwamba katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri, iliidhinishiwa jumla ya Tshs.6,701,965,358.00/= kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji na uboreshaji wa miundombinu katika Sekta ya Elimu, Afya, Utawala, Kilimo na Mifugo ambapo mapato ya Ndani ni Tshs.749,285,681/=, Serikali Kuu ni Tshs.1,950,000,000.00, TASAF Tshs.1,876,982,000/=, SEQUIP

Tshs.985,200,000/=, Mfuko wa Jimbo (CDCF) ni Tshs.55,415,000/=, LANES Tshs.64,510,000/=, EP4R Tshs.693,163,000/=, Maabara Tshs.150,000,000/=, na Maboma Tshs. 225,000,000/= fedha hizo hazijumuishi fedha za Elimu bila malipo na fedha za EGPAF, BASKET na UNICEF.

Hadi kufikia tarehe 31 Septemba, 2021 kiasi cha Tshs.394,681,000/= kimetolewa, kati ya fedha hizo Tshs.69,681,000/= ni fedha za TASAF na Tshs.325,000,000/= ni fedha zilizotolewa nje ya bajeti zikiwemo fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya Tshs.250,000,000/=, ujenzi wa madarasa 4 katika Shule za Sekondari Tshs.50,000,000/= na fedha za chanjo ya UVIKO19 Tshs.25,000,000/=.

Aidha, alieleza kwamba zimetengwa Tshs.164,056,276.20/= za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi mbalimbali inayotekeliza kwa fedha za mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na ukarabati wa Kituo cha Afya.

Kwa kipindi cha mwezi Julai-Septemba 2021/2022 Halmashauri kupitia Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji imetekeliza shughuli zifuatazo;

- i. Kuratibu maandalizi ya zoezi la Sensa ya Kitaifa ya watu na makazi itakayofanyika mwaka 2022 ikiwa ni pamoja na kuunda kamati ngazi ya Wilaya, Kata, Vijiji na Vitongoji kwa mujibu wa maelekezo kutoka OR-TAMISEMI.
- ii. Kuratibu zoezi la maandalizi na uchambuzi wa taarifa za maombi ya fedha za miradi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kuwasilisha wizara ya fedha na OR-TAMISEMI.
- iii. Kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekeliza ngazi ya Vijiji na Kata ikiwemo ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri, Ujenzi wa madarasa mawili, matundu ya vyoo Shule ya Sekondari Mkuu na ujenzi wa wodi tatu Hospitali ya Wilaya.
- iv. Kuratibu na kuandaa taarifa ya hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.
- v. Kuratibu ukusanyaji wa taarifa za miradi itakayotekeliza katika ngazi ya Vijiji na Kata.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji miradi Robo ya kwanza.
- vii. Kuratibu maandalizi ya bajeti iliyovuka mwaka.

Alimalizia kwa kuwaeleza wajumbe kuwa kumekuwa na changamoto ya kucheleta kutolewa kwa fedha kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji wa miradi iliyokuwa imekusudiwa na hivyo kuwepo kwa uwezekano wa miradi hiyo kutekelezwa nje ya muda uliokusudiwa na kwa muda mrefu bila kutekelezwa.

Aidha miradi iliyobuliwa na wananchi kwenye maeneo yao kukaa kwa muda mrefu bila kuendeleza kutokana na mwitikio mdogo wa jamii husika kuiendeleza miradi hiyo kwa kuchangia rasilimali mbalimbali na badala yake miradi hiyo kutegemea kuendeleza kwa fedha za Serikali tu ambayo inakuwa haitoshelezi kutekelezza miradi hiyo kwa wakati mmoja. Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

Jengo la Ghorofa Kata ya Mamsera

Katika kujadili taarifa hiyo Afisa Mipango na Takwimu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwaeleza wajumbe kuwa katika Kata ya Mamsera litajengwa jengo la ghorofa kwa ajili ya Shule mpya ya Sekondari katika eneo la Shule ya Msingi Kiungu ambapo Serikali iliahidi kutoa Tshs.600,000,000/=.

Mjumbe mmoja alieleza kuwa Halmashauri inapokea fedha nyingi hivyo alishauri kuwa kuna haja ya kuboresha baadhi ya Vitengo kama kile cha Ukaguzi wa Ndani ili kuepuka maswali mengi yanayoweza kuulizwa baadae.

Uzalishaji Bora wa Miche ya Parachichi

Mjumbe mmoja alishauri kuwa ni vizuri kuzalisha miche ya parachichi kwenye bustani ya Halmashauri ili kupunguza gharama za kununua miche hiyo. Aidha, alishauri kwamba litafutwe eneo katika msitu wa nusu Maili kwa ajili ya kupanda miche hiyo ya parachichi kwa kuwa bei ya zao hilo ni nzuri.

Afisa Mipango na Tkwimu alitolea ufanuzi hoja hiyo ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa Tshs.900,000,000/= ilitengwa kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya parachichi katika bustani ya Halmashauri kwa ajili ya kusambaza katika maeneo mbalimbali ya Wilaya.

Aidha, mjambe mmoja alieleza kuwa ana wasiwasi ikiwa wataalam wakiagizwa wakaoteshe zao hilo katika msitu wa Halmashauri kwani eneo hilo halina ulinzi wa kutosha, hivyo yatakapokuwa tayari yataliwa yote na Halmashauri isipate chochote.

Zahanati ya Mfuruwashen na Shimbi

Mjambe mmoja alieleza kuwa fedha hazijatolewa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya Mfuruwashen na Shimbi hivyo aliwasilisha ombi lake la kupatiwa mba kwa ajili ya zahanati ya Mfuruwashen kwani kuna mfadhili aliyepatikana kwa ajili ya kuendeleza ujenzi katika zahanati hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji akitolea ufanuzi hoja hiyo alimwomba mjambe huyo kuwasiliana na Mtendaji wake wa Kata ili afanye Mawasiliano na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

Mjambe mmoja alihoji kutaka kujua taarifa za WDC zinazowasilishwa kama zinapitiwa kwani Ofisi ya kata ya Mraokeryo ipo katika hali ya hatari.

Mkurugenzi Mtendaji akitolea ufanuzi hoja hiyo aliwaeleza wajumbe kuwa hoja hiyo imepokelewa na itafanyiwa kazi.

AGENDA; NA. 27/2021/2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI – SEPTEMBER 2021/2022.

Mweka Hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya Fedha za Halmashauri kwa kipindi cha mwezi Julai-Septemba 2021/2022 na kueleza kuwa kwa kipindi hicho Halmashauri ilipanga kukusanya jumla ya Tshs. 630,348,943/= kwa mchanganuo ufuatao;

Mapato ya Ndani	Tshs. 610,226,193
Fidia ya Ruzuku	Tshs. 20,122,750
Jumla	Tshs. 630,348,943

Hadi kufikia tarehe 30.09.2021 Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya Tshs.540,485,039/= sawa na asilimia 85.7 ya lengo la mwezi Julai - Septemba 2021 na 21.4 ya lengo la mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa mchanganuo ufuatao;

Mapato ya Ndani	Tshs. 540,485,039
Fidia ya Ruzuku	Tshs. 0
Jumla	Tshs. 540,485,039

Kwa kipindi cha mwezi Septemba 2021 Halmashauri ilipanga kukusanya katika vyanzo vyake vya mapato jumla ya Tshs. **210,116,314** kwa mchanganuo ufuatao;

Mapato ya Ndani	Tshs. 203,408,731
Fidia ya Ruzuku	Tshs. 6,707,583
Jumla	Tshs. 210,116,314

Hata hivyo Halmashauri kuitia vyanzo vyake vya ndani katika mwezi Septemba 2021 imeweza kukusanya jumla ya **Tshs 168,088,207/=** ikiwa ni sawa na asilimia 80 ya lengo la mwezi Agosti 2021.

Mapato ya ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo (PE na OC).

Kwa upande wa ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo Halmashauri iliidhinisha kupokea jumla ya **Tshs. 30,688,508,795** katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa mchanganuo ufuatao;

Mishahara	Tshs. 28,813,452,000
Matumizi mengineyo	Tshs. 1,875,056,795
Jumla	Tshs. 30,688,508,795

Kwa kipindi cha mwezi Julai - Septemba 2021 Halmashauri ilipanga kupokea jumla ya **Tshs.7,672,127,199/=** kwa mchanganuo ufuatao;

Mishahara	Tshs. 7,203,363,000
Matumizi mengineyo	Tshs. 468,764,199
Jumla	Tshs. 7,672,127,199

Hadi kufikia tarehe 30.09.2021 Halmashauri imepokea jumla ya **Tshs.7,672,326,500/=** sawa na asilimia 102 ya lengo la mwezi Julai - Septemba 2021 na asilimia 25.5 ya lengo la mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mapato ya Miradi ya Maendeleo na Wahisani mbalimbali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwa upande wa miradi ya Maendeleo na wahisani mbalimbali, Halmashauri ilikisia kupokea jumla ya **Tshs. 10,318,144,181/=** kutoka kwa wachangiaji mbalimbali.

Katika kipindi cha mwezi Julai - Septemba 2021 Halmashauri ilipanga kupokea jumla ya **Tshs.2,579,536,045/=** kutoka Serikali Kuu na wachangiaji mbalimbali.

Hadi kufikia tarehe 30.09.2021 Halmashauri imepokea jumla ya **Tshs. 760,096,469/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na 29% ya lengo la mwezi Julai-Septemba 2021 na asilimia 7 ya lengo la mwaka wa fedha 2021/2022.

MATUMIZI

Matumizi ya Vyanzo vya Ndani na Ruzuku ya Fidia.

Kwa upande wa matumizi ya vyanzo vya ndani na ruzuku ya fidia Halmashauri iliidhinisha kutumia jumla ya **Tshs.2,521,395,772** kwa Idara mbalimbali za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Katika kipindi cha mwezi Julai-Septemba 2021 Halmashauri ilikisia kutumia jumla ya **Tshs.630,348,943/=** kutoka vyanzo vyake vya ndani na ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu.

Hadi kufikia tarehe 30/09/2021 Halmashauri imetumia jumla ya **Tshs.544,643,662/=** ikiwa ni sawa na asilimia 86.4 ya lengo la mwezi Julai-Septemba 2021 na asilimia 21.6 ya lengo la mwaka wa fedha 2021/2022.

Matumizi ya Ruzuku ya Mishahara na Matumizi mengineyo.

Katika mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Halmashauri ilikisia kutumia kiasi cha **Tshs.30,688,508,795** kwa ajili ya kugharamia mishahara ya watumishi wake na matumizi mengineyo (OC).

Katika kipindi cha mwezi Julai - Septemba 2021 Halmashauri ilikisia kutumia jumla ya **Tshs.7,672,127,199/=** kutokana na ruzuku ya Serikali.

Hadi kufikia tarehe 30.09.2021 Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs.7,289,802,679/=** kwa ajili ya kulipia gharama za mishahara ya watumishi na matumizi mengineyo sawa na 93% ya lengo la mwezi Julai-Septemba 2021 na asilimia 24 ya lengo la mwaka wa fedha 2021/2022.

Matumizi ya Miradi ya Maendeleo na Wahisani mbalimbali.

Katika kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo, Halmashauri ilikisia kutumia kiasi cha **Tshs.10,318,144,181/=** kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Katika kipindi cha mwezi Julai-Septemba 2021/2022 Halmashauri ilikisia kutumia jumla ya **Tshs.2,579,536,045/=** kutokana na ruzuku ya miradi ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu na wahisani mbalimbali.

Hadi kufikia tarehe 30.09.2021 Halmashauri imetumia jumla ya **Tshs.588,886,614/=** sawa na asilimia 23 ya lengo la mwezi Julai-Septemba 2021/2022 na asilimia 5.7 ya lengo la mwaka wa Fedha 2021/2022.

**HALI YA FEDHA KAMA ILIVYO KATIKA VITABU VYA HALMASHAURI YA
WILAYA YA ROMBO TAREHE 30/07/2021**

SN	JINA LA AKAUNTI	SALIO LA FEDHA KATIKA VITABU VYA (HW) ROMBO
1	Akaunti ya Maendeleo iliyopo Benki Kuu (LGAS- Development Account)	74,505,161.27
2	Akaunti ya Maendeleo iliyopo Benki Kuu	336,503,391.82
3	Akaunti ya Elimu iliyopo Benki Kuu (LGAS- Education sector Account)	231,613,000.00
4	Akaunti ya Mfuko Mkuu iliyopo Benki Kuu (LGAS- General Fund Account)	1,153,704.50
5	Akaunti ya Afya iliyopo Benki Kuu (LGAS-Health Sector Account)	9,414,745.57
6	Akaunti ya Amana iliyopo Benki Kuu (LGAS- Misc Deposit Account)	25,579,749.41
7	Akaunti ya Matumizi ya kawaida iliyopo Benki Kuu (LGAS-other Charges Account)	1,000,000.00
8	Akaunti ya mishahara iliyopo Benki Kuu) (LGAS- Personal Emolument Account)	-
9	Akaunti ya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu iliyopo Benki Kuu	6,668,053.00
10	Akaunti ya Amana iliyopo NMB Misc Deposit Account)	635,636.16
11.	Akaunti ya Mapato iliyopo NMB Benki (RDC – Revenue Cash Account)	9,545,727.48
12.	Akaunti ya Mapato iliyopo CRDB Benki (RDC – Revenue Cash Account)	21,892,919.70
13.	Women Youth Disability Rombo DC NMB	-
	JUMLA	718,512,088.9

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

Ada ya Kukodisha Mashamba

Mjumbe mmoja alihoji kutaka kujua ada ya kukodisha mashamba huwa inakusanywa wakati gani.

Afisa Ardhi na Maliasili kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji alitolea ufanuzi hoja hiyo ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa ada hiyo ilipangwa kukusanywa katika kipindi cha mwezi Februari 2022.

Mjumbe mmoja alieleza kuwa anakubaliana na majibu ya wataalam. Hata hivyo alieleza kuwa anaona ufanisi wake utakuwa ni mdogo kwa sababu wakati mwengine huwa wana tabia ya kuwafuata wakulima mashambani hivyo mahindi yakishakuwa makubwa wakulima hao hawatapatikana na kuwa itabidi kusubiri hadi mwezi Machi kuona Makusanyo yaliyofanyika katika kipindi cha mwezi Februari.

Mjumbe mmoja alieleza kuwa kama wakulima hao wapo shambani katika kipindi cha mwezi Oktoba 2021 ndiyo kipindi kizuri cha kukusanya ada kwani ifikapo Februari 2022 mazao yatakuwa yamesharefuka na hakuna atakayepatikana shambani na wengine watakuwa wamevuna.

Afisa Ardhi na Maliasili kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji alitolea ufanuzi hoja hiyo ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa ada hiyo inakusanya wa Februari kwa maana ya kukusanya kwa mwaka mzima kwani mashamba hayo yanakodishwa kwa mwaka mmoja mmoja na itakapofika kipindi hicho mashamba hayo yatagawiwa tena upya. Aidha alieleza kuwa kama kuna maelekezo mengine Idara ipo tayari kwa utekelezaji.

Mjumbe mmoja alieleza kuwa lengo ni kupatikana kwa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022 na ndiyo maana kumekuwa na hofu ya ukusanyaji katika kipindi cha mwezi Februari kwa kuwa kwa miaka ya nyuma ada hiyo ilikuwa inakusanya katika kipindi cha mwezi Oktoba ambacho ndiyo mwafaka zaidi. Aliendelea kueleza kuwa kuna wakulima waliogawiwa mashamba katika kipindi hicho cha mwezi Februari na kuna wale wanaoendelea kulima mashamba hayo kwa muda mrefu.

Afisa Ardhi na Maliasili kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji alitolea ufanuzi hoja hiyo ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa hoja hiyo imepokelewa kwa ajili ya utekelezaji.

AZIMIO

Wakulima wanaolima kuanzia miaka ya nyuma waendelee kulipa ada ya kukodisha mashamba.

Ushuru wa Masoko

Mjumbe mmoja alihoji kutaka ufanuzi juu ya akina mama wanaobeba ndizi na kuzipeleka sokoni na kutozwa Tshs.100/=, pia alitaka ufanuzi wa tozo kwa wafanyabiashara wanaonunua ndizi kwa magari.

Kaimu Mweka Hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji alitolea ufanuzi hoja hiyo na kuwaeleza wajumbe kuwa kuhusiana na tozo kwenye ndizi wafanyabiashara wanatozwa kwa gari Tshs.15,000/= na wale wanaopanga pia wanatozwa Tshs.100/=.

AGENDA; NA. 28/2021/2022: TAARIFA YA MADENI YA WAZABUNI HADI SEPTEMBA 2021.

Kaimu Mweka Hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya madeni ya wazabuni hadi Septemba 2021 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo kufikia mwezi septemba 2021 ilikuwa na deni la jumla ya kiasi cha Tshs.304,252,120.50. aliendelea kueleza kuwa deni hilo ni la muda mrefu ambalo limekaa kwa zaidi ya miezi 24. Aidha aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imeweka mikakati mbalimbali kwa ajili ya kupunguza madeni yake kama ifuatavyo;

- i. Kuwasilisha changamoto za uwepo wa madeni ya muda mrefu ya Halmashauri kila ifikapo mwisho wa mwaka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).
- ii. Kutenga katika bajeti ya kila mwaka kiasi kidogo kwa ajili ya kupunguza madeni ya muda mrefu ambapo kwa mwaka huu Halmashauri imeshalipa kampuni ya Tilisho kiasi cha Tshs.10,250,000 na Johana 8,320,000.
- iii. Kufanya malipo kwa wazabuni kwa kutumia fedha za bakaa ambapo kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Halmashauri imeilipa Kampuni ya Elerai Tshs.192,904,447.
- iv. Kufanya mapitio ya bajeti kila ifikapo katikati ya mwaka wa Fedha ambapo mafungu ambayo hayajatumika hubadilishiwa matumizi na kuelekezwa katika kupunguza madeni . aliendelea kueleza kuwa Halmashauri inatarajia kufanya mapitio ya bajeti ifikapo mwezi Desemba 2021.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe hawakuridhika taarifa hiyo kwa kuwa haijaka sawa na maagizio yaliyotolewa hivyo waliagiza taarifa hiyo ikaandaliwe upya na kuwasilishwa kwenye kikao kijacho.

AGENDA; NA. 29/2021/2022: TAARIFA YA MANUNUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2021/2022.

Kaimu Afisa Manunuzi Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya manunuzi yaliyofanyika kwa robo ya kwanza (Julai-Septemba) 2021/2022 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa katika kipindi hicho Halmashauri imefanya manunuzi kwa njia ya LPO yenye thamani ya jumla ya Tshs.73,221,889.86 kwa mchanganuo ufuatao;

Mwezi Agosti Tshs.21,193,295.36

Mwezi Septemba Tshs.52,028,594.50

Jumla Tshs.73,221,889.86

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuipitisha.

AGENDA; NA. 30/2021/2022: TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2021/2022.

Mkaguzi wa ndani aliwasilisha taarifa ya ukaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa kuna hoja 9 za Ukaguzi uliopita, kati ya hizo 1 imetekelizwa na 8 bado hazijatekelezwa. Aliendelea kueleza kuwa katika ukaguzi wa robo ya nne kulikuwa na hoja 14 ambapo kati ya hizo 4 zimejibowi na 10 bado hazijapata majibu. ambazo zote hazijafungwa.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe waliagiza kuwa yale yaliyoelekezwa na Mkaguzi wa ndani yazingatiwe.

AZIMIO

Wataalam wafanyie kazi yale yaliyoelekezwa na Mkaguzi wa Ndani.

AGENDA; NA. 31/2021/2022:TAARIFA YA KESI MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI-SEPTEMBA 2021.

Afisa Sheria kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya Kesi mbalimbali za Halmashauri kwa kipindi cha mwezi Julai-Septemba 2021 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa kuna idadi ya kesi tisa (09) za madai kama ifuatavyo;

1. Shauri Na. 136/2015; Francis Mathias Massawe dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Magreth Peter Ngassa (Msimamizi wa mirathi ya marehemu Peter Ngassa Mmbando) na M/S Independence Agencies & Court Brokers.

Hili ni shauri ambalo mwombaji amerudisha kwenye baraza hilo kutokana na amri ya Mahakama Kuu kwenye Rufaa Na. 2/2015 kuwa shauri hili linahitajika kurudi kwa ajili ya kusikilizwa upya. Shauri hili linahusu maombi ya kulipwa fidia ya shamba la mdai lenye hekari sita lenye thamani ya million arobaini na tano (45,000,000) kwa ajili ya maendelezo aliyoyafanya kwenye Kitalu namba 231 block A na shilingi milioni tano (5,000,000) ili afanye marekebisho ya uharibifu uliofanyika. Pia ameomba Mahakama alipwe shilingi milioni thelathini na mbili na laki nne (32,400,000) kama fidia ya madhara aliyoyapata kwa kipindi cha miezi saba ambapo alishindwa kupata kipato kwenye ekari hizo sita.

Shauri hili limerudishwa kwenye Baraza kwa amri ya Mahakama Kuu kupitia rufaa Na; 2/2015 kwa ajili ya kusikilizwa upya.

Shauri linaendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa Mjibu Maombi Na.3 tarehe 01/11/2021.

2. Shauri la Ardhi Na. 07/2020; Apolinary France Shirima (muombaji wa 1) na Anna Apolinary na Sigimanta Boniface Asenga (mjibu maombi Na 2).

Hili ni shauri ambalo waombaji wamepeleka maombi katika Baraza la ardhi na Nyumba Wilaya wakidai kuingiliwa kwenye eneo hilo na Kijiji cha Kirwa ambapo Kijiji hicho kimempangisha Sigimanta Boniface Asenga. Hivyo wameomba Baraza kumtaja kuwa yeye ndio mmiliki halali wa eneo hilo ambalo lina ukubwa wa mita 25x7 lenye makadirio ya thamani ya shilingi 8,000,000.

Shauri limepangwa kuanza kusikilizwa upande wa wadai tarehe 17/11/2021.

3.Mgogoro wa Kazi Na.CMA/KLM/RMB/M/240/2020; Godlove M. Francis dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Shauri hili ni la maombi ya kutaka kulipwa nauli ya kurudishwa kwao baada ya kufukuzwa kazi pamoja na madai yake ya kutolipwa malimbikizo ya mishahara baada ya kupanda cheo mwaka 2010 hadi 2012.

Gharama za kujikimu kwa kutolipwa tangu alipofukuzwa kazi hadi uamuizi utakapotolewa.

Mwamuizi (Arbitrator) ampanga kusikiliza pingamizi la awali kwa njia ya maandishi (by way of written submissions) na hivyo uamuizi utatolewa tarehe 25.10.2021.

4. Shauri la Madai Na.15/2021; Halmashauri ya Wilaya ya Rombo dhidi ya Angel Assey.

Hili ni shauri la madai ambalo lipo Mahakama ya Mwanzo Mkuu ambapo mdai (Halmashauri ya Wilaya ya Rombo) anamdai Mdaiwa Angel Assey kiasi cha Tshs.1,615,000/= ikiwa ni madai ya kodi ya pango la mgahawa na deni la leseni ya biashara.

Shauri limetolewa uamuizi tarehe 27.08.2021 kuwa Mdaiwa ailipe Halmashauri Tshs.1,615,000/. Aidha mali na vifaaa vyote vilivyoachwa na Mdaiwa kwenye mgahawa vipigwe mnada kufidia deni analodaiwa.

5. Mapitio ya kazi (Labour Revision) Na.21/2021 Hamis Haji Mfinanga dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hili ni shauri la maombi ambalo lipo Mahakama Kuu ambapo mdai anaomba Mahakama ifanye mapitio ya Tuze ya Tume ya usuluhishi na uamuizi katika mgogoro wa kikazi Na.CMA/KLM/RMB/42/2021 iliyotolewa tarehe 11.05.2021 na hivyo kutoa amri ya kuifuta kutokana na makosa kadhaa ya Kisheria.

Shauri limepangwa kusikilizwa kwa njia ya maandishi (by way of written submissions) na uamuizi umepangwa kutolewa tarehe 15.10.2021.

6. Mapitio ya kazi (Labour Revision) Na.32/2021 Godlove Mandia dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hili ni shauri la maombi ambalo lipo Mahakama Kuu ambapo mdai anaomba Mahakama ifanye mapitio (Revision) ya uamuizi uliotolewa tarehe 11/05/2021 na Tume ya Usuluhishi na Uamuizi Moshi ambayo ilitupilia mbali maombi yake kufungua mgogoro wa kazi nje ya muda wa Kisheria.

Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 11.10.2021.

7. Shauri la Madai Na.27/2021; Halmashauri ya Wilaya ya Rombo dhidi ya kikundi cha Motamburu Young Enterpreneur na Alphonce Elias Shirima.

Hili ni shauri la madai ambalo lipo Mahakama ya Mwanzo Mkuu ambapo Halmashauri katika kipindi cha mwaka 2019/2020 ilikipatia kikundi (Mdaiwa Na. 1) mkopo wa kiasi cha Tshs.8,000,000/= hivyo kikundi kinadaiwa fedha za marejesho ya Tsh. 5,332,000/= ambazo bado hazijalipwa. Faini ya Tshs.2,000,000.00 ikiwa ni asilimia 25 ya thamani ya mkopo kwa ucheleweshaji kwa mujibu wa mkataba ulioingiwa kati ya Halmashauri. Maombi ya kukamata na kuuza (attachment & sale) ya mali za Mdaiwa Na.2 ambaye alidhamini kikundi husika.

Shauri limepangwa kuanza kusikilizwa tarehe 12.10.2021.

8. Shauri la Madai Na.28/2021; Halmashauri ya Wilaya ya Rombo dhidi ya kikundi cha Sinai Group na Hawa Bakari.

Hili ni shauri la madai ambalo lipo Mahakama ya Mwanzo Mkoo ambapo Halmashauri katika kipindi cha mwaka 2019/2020 ilikipatia kikundi (Mdaiwa Na. 1) mkopo wa kiasi cha Tshs.10,000,000/= hivyo kikundi kinadaiwa fedha za marejesho ya Tsh. 8,500,000/= ambazo bado hazijalipwa. Faini ya Tshs.2,500,000.00 ikiwa ni asilimia 25 ya thamani ya mkopo kwa ucheleweshaji kwa mujibu wa mkataba ulioingiwa kati ya Halmashauri. Maombi ya kukamata na kuuza (attachment & sale) ya mali za Mdaiwa Na.2 ambaye alidhamini kikundi husika. Shauri limepangwa kuanza kusikilizwa tarehe 12.10.2021.

9 Shauri la Madai Na.26/2021; Halmashauri ya Wilaya ya Rombo dhidi ya kikundi cha Kimboma Group na Bilasi Abdalah Tesha.

Hili ni shauri la madai ambalo lipo Mahakama ya Mwanzo Mkoo ambapo Halmashauri katika kipindi cha mwaka 2019/2020 ilikipatia kikundi (Mdaiwa Na. 1) mkopo wa kiasi cha Tshs.4,500,000/= hivyo kikundi kinadaiwa fedha za marejesho ya Tsh. 4,500,000/= ambazo bado hazijalipwa. Faini ya Tshs.1,125,000.00 ikiwa ni asilimia 25 ya thamani ya mkopo kwa ucheleweshaji kwa mujibu wa mkataba ulioingiwa kati ya Halmashauri. Maombi ya kukamata na kuuza (attachment & sale) ya mali za Mdaiwa Na.2 ambaye alidhamini kikundi husika. Shauri limepangwa kuanza kusikilizwa tarehe 12.10.2021.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuipitisha.

AGENDA NA. 32/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KERO ZA WANANCHI KWA KIPINDI CHA JULAI-SEPTEMBA 2021/2022

Afisa Kero kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kero za wananchi kwa kipindi cha Julai-Septemba 2021/2022 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa kwa kipindi tajwa hapo juu Halmashauri ilipokea kero 12 (kero za Maji 03, Ardhi 04, Maendeleo ya Jamii 01, Utumishi na Utawala 01 na nyinginezo 03) kutoka ngazi ya Vijiji, Kata na Wilaya. Aliendelea kueleza kuwa jumla ya kero 09 zimepatiwa ufumbuzi na kero 03 zilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.alimalizia kkwa kueleza taarifa ya kero 01 ambayo iliwasilishwa na haikupatiwa ufumbuzi kwa kipindi cha Aprili-Juni 2020/2021 ambapo alieleza kuwa utekelezaji wake ulikuwa umeshafanyika.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

AGENDA NA. 33/2021/2022: TAARIFA YA UKARABATI NA UJENZI WA KITOO CHA AFYA MKUU.

Afisa mipango, Takwimu na Ufutiliaji niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya ukarabati wa kituo cha Afya Mkoo ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imepokea fedha nje ya bajeti kiasi cha Tshs.250,000,000/= kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya katika Tarafa ya Mkoo. Aliendelea kueleza kuwa Halmashauri imefikia uamuza wa kuomba kibali cha kukarabati jengo la Ofisi ya Mkurugezi Mtendaji badala ya kujenga jengo jipya la wagonjwa wa nje (OPD) kwa kuwa kwa sasa Halmashauri inajenga jengo la Utawala ambalo lipo katika hatua ya mwisho ya ujenzi kwani litakuwa na ofisi za kutosha kila Idara na Vitengo. Katika Tarafa ya Mkoo hakuna eneo linalokidhi vigezo vya ujenzi wa kituo cha Afya. Aidha tarafa ya mkoo kutokuwa na kituo cha Afya.

Vile vile alieleza kuwa majengo mengine yanayohitajika kujengwa kwa fedha zilizotolewa na Serikali Kuu ni kama ifuatavyo;

- i. Maabara Tshs.98,327,700/=
- ii. Kichomea taka Tshs. 4,671,600/=
- iii. Jengo la Upasuaji Tshs.143,219,340/=

Alimalizia kwa kueleza kuwa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) litafanyiwa ukarabati kwa kutumia fedha za mapato ya ndani Tshs.94,025,628/=

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

**AGENDA NA. 34/2021/2022: TAARIFA YA MAPENDEKEZO YA UTEUZI WA
WENYEVITI NA MAKATIBU WA MABARAZA YA KATA**

Kaimu Afisa Sheria kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya mapendekezo ya uteuzi wa Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza ya Kata ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa Menejimenti imepitia mapendekezo yaliyowasilishwa na Kata zifuatazo kuwa wafuataao wateuliwe kuwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Kata katika kata hizo;

S/ N	KATA	MAJINA	UMRI	JINSI	KIJIJI ANACHOISHI	SHUGHULI ANAZOJISHUGHULISHA NAZO
1	Tarakea Motamburu	Barnabas Mchomba	48	Me	Mbomai	Kilimo
2	Chala	Rosada Lyakurwa A.	60	Ke	Kidondoni	Kilimo
3	Ushiri Ikuini	Pascal Masaule Mroso	64	Me	ushiri	Kilimo

Aidha aliwaeleza wajumbe kuwa Menejimenti imepitia mapendekezo yaliyowasilishwa na Kata zifuatazo kuwa wafuataao wateuliwe kuwa Makatibu wa Mabaraza ya Kata katika kata hizo;

S/ N	KATA	MAJINA	UMRI	JINSI	KIJIJI ANACHOISHI	SHUGHULI ANAZOJISHUGHULISHA NAZO
1	Tarakea Motamburu	Teddy Mushi	36	Ke	Mbomai	Afisa Mifugo
2	Chala	Kerbin Mongi		Ke	Kidondoni	Afisa Elimu Kata
3	Ushiri Ikuini	Farida Hatim Janowalah	36	Ke	ushiri	Afisa Maendeleo ya Jamii

Wajumbe walipokea tarifa hiyo na kuijadili.

Baada ya majadiliano ya kina wajumbe walipitisha taarifa hiyo.

**AGENDA NA. 35/2021/2022: TAARIFA YA MZABUNI ALIYESHINDA ZABUNI YA
UZOAJI TAKA NGUMU ZABUNI NA.LGA/044/HQ/2021/2022/NC/07 LOT 1 & LOT 2
NA ZABUNI YA UKUSANYAJI USHURU WA MAEGESHO STENDI YA MKUU,
HOLILI NA TARAKEA**

Kaimu Afisa manunuzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwaeleza wajumbe kuwa Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo katika kikao chake cha tarehe 23/09/2021 ilitoa zabuni ya uzoaji taka Ngumu Wilaya ya Rombo kwa mzabuni JOHANA TRADERS S.L.P 10316 MOSHI.

Aidha Bodi hiyo katika kikao chake cha tarehe 23/09/2021 ilitoa zabuni ya ukusanyaji Ushuru wa maegesho ya magari katika stendi ya Mkuu, Holili na Tarakea kwa mzabuni EAC GROUP (T) LTD S.L.P 60206 DAR ES SALAAM kwa gharama ya Tshs.11,655,00/= kwa mwezi. Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe walieleza kwamba tangazo la zabuni ya uzoaji taka Ngumu halikuonekana kwenye mbao za matangazo, hivyo waliagiza kuwa wakati mwingine matangazo ya zabuni yawe yanabandikwa kwenye mbao za matangazo.

**AGENDA NA. 36/2021/2022: TAARIFA YA MPANGO WA KUINUA UCHUMI NA
HUDUMA ZA KIJAMII BAADA YA UVIKO 19 (TANZANIA COVID 19 SOCIO-
ECONOMIC RECOVERY AND RESPONSE PLAN (TCRP)**

Afisa Mpango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya mpango wa kuinua uchumi na huduma za kijamii baada ya UVICO 19 ambapo aliwaeleza

wajumbe kuwa wilaya ya Rombo ni mionganoni mwa Halmashauri zilizopo kwenye mpango maalum wa kupitiwa fedha za miradi ya maendeleo chini ya mapambano dhidi ya UVIKO 19. Aliendelea kueleza kuwa katika mpango huo sekta za kipaumbele ni Elimu na Afya, ambapo katika Sekta ya Elimu Msingi na Sekondari imepangiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 44 ambapo kila darasa limepangiwa fedha Tshs.20,000,000/= kwa mchanganuo ufuatao;

- i. Elimu Msingi Vyumba viwili vya madarasa Tshs. 40,000,000/=
- ii. Elimu sekondari vyumba 42 vya madarasa Tshs.840,000,000/=

Aidha alieleza kuwa katika sekta ya afya Halmashauri imepangiwa fedha kwa ajili ya

- i. Emergence Medical Department (Casuality) Tshs.300,000,000/=
- ii. Ununuzi wa mitambo ya mionzi Tshs.420,000,000/=
- iii. Gari moja la wagonjwa (Ambulance).

Alimalizia kwa kueleza kuwa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa Tshs.880,000,000/ zimeshapokelewa kwenye akaunti ya maendeleo ya miradi (Development Exchecq).

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili.

Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe walishukuru kwa kupokea fedha hizo.

Mjumbe mmoja aliomba wataalam wakajenge hoja watakapoenda kwenye kikao Mkoani ili shule za ghorofa ili ziweze kupitiwa pia fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo ya ghorofa kwani majengo hayo hayapo katika hali salama.

Wajumbe waliagiza kwamba manunuvi ya vifaa vya ujenzi yafanyike kwa wakati ili kuepukana na changamoto ya upatikanaji wa vifaa hivyo.

AGENDA; NA. 37/2021/2022:- TAARIFA YA VIKUNDI VILIVYOPITISHWA NA KAMATI YA MIKOPO ROBO YA KWANZA JULAI-SEPTEMBA 2021/2022

Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya vikundi vilivyopitishwa na Kamati ya Mikopo robo ya kwanza Julai-Septemba 2021/2022 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa katika kipindi hicho Halmashauri ilitoa mikopo yenye thamani ya Tshs.104,182,606.60/= kutoka mapato ya ndani (Ownsource) kiasi cha Tshs.39,507,649/= na fedha kutoka mfuko wa mzunguko (Revolving) Tshs.64,674,958/= kwenda kwenye vikundi vya Vijana ,Wanawake na Watu Wenye Ulemavu.

Maombi yaliyowasilishwa kwa kipindi cha Julai-Septemba 2021/2022 ni kama ifuatavyo;

Vikundi vitano (5) vya Vijana	- Tshs.76,000,000/=
Vikundi thelathini na nane (38) vya Wanawake	-Tshs.415,397,700/=
Vikundi sita (6) vya Watu Wenye Ulemavu	-Tshs. 16,500,000/=
Jumla	-Tshs.519,897,700/=

Vikundi vilivyopitishwa na Kamati ya Mikopo ni kama ifuatavyo;

Vikundi viwili (2) vya Vijana	-Tshs.27,000,000.00
Vikundi saba (07) vya Wanawake	-Tshs.41,673,042.64
Vikundi sita (6) vya Watu Wenye Ulemavu	-Tshs.20,836,521.32
Jumla	-Tshs.89,449,563.96

Alimalizia kwa kueleza kuwa kiasi cha fedha Tshs.14,673,042.64 iliyokuwa imebaki kwa vikundi vya Vijana itatolewa baada ya kamati ya mikopo Wilaya kujiridhisha na shughuli wanazofanya.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili.

Katika kujadili taarifa hiyo mjumbe mmoja alihoji kama maboresho ya taarifa hiyo yameshafanyika kama ambayo Kamati ya Elimu, Afya na Maji ilivyoagiza.

Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii alitolea ufanuzi hoja hiyo ambapo aliwaeleza wajumbe kwamba maboresho hayo yameshafanyika kama kamati ilivyoagiza.

Baada ya majadiliano ya kina wajumbe walipitisha taarifa hiyo.

AGENDA; NA. 38/2021/2022:- TAARIFA MBALIMBALI.

• Taarifa ya Eneo lililokuwa linamiliikiwa na ITV

Kaimu Mkurugenzi aliwaeleza wajumbe kuwa eneo lililokuwa linamiliikiwa na ITV limerejeshwa kwa Halmashauri hivyo aliwaomba wajumbe kuridhia ili watembelee eneo hilo mara baada ya kikao.

Wajumbe walishauri itafutwe siku maalum ili kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango itembelee eneo hilo.

Aidha waliagiza taarifa iandaliwe kwa maandishi ili iwasilishwe kwenye kikao kijacho cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

AZIMIO

Taarifa iandaliwe kwa maandishi ili iwasilishwe kwenye kikao kijacho cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

• Tangazo la Quarantine ya Kimeta (Anthrax)

Kaimu Afisa Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi aliwasilisha tangazo la la Quarantine ya Kimeta (Anthrax) ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa maeeneo ya Kata ya Mamsera, Mahida na Chala yameambukizwa ugonjwa wa kimeta. Aliendelea kueleza kuwa ni marufuku kuingiza, kutoa au kupitishaNg'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe au mazao yatokanayo na wanyama hao kwenye maeneo yaliyotajwa bila idhini ya maandishi kutoka kwa Daktari wa mifugo wa Wilaya. Mnyama yoyote atakayekufa azikwe bila kuchunwa chini ya uangalizi wa Daktari wa Mifugo na kuhakikisha Mifugo inapatiwa chanjo ya kuzuia ugonjwa wa Kimeta. Alihitimisha kwa kuwaeleza wajumbe kuwa zuio hilo litaanza rasmi tarehe 23.10.2021.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili.

Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe walieleza kuwa ni vizuri wananchi wazingatie masharti yaliyoelezwa katika tangazo la zuio.

AGENDA; NA. 39/2021/2022:- KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kikao na kuwataka wataalam wa Halmashauri kuyafanya kazi mambo yote yaliyoazimiwa kisha alifunga kikao saa 7:40 mchana.

U M E T H I B I T I S H W A.

Katibu

Judith P. Mahende

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)

Mwenyekiti

Gilbert A. Tarimo

MWENYEKITI WA HALMASHAURI

ROMBO.

ROMBO.

TAREHE 26.11.2021.....